


**YOTE UNAYOHITAJI
KUJUA KUHUSU
KUPIMWA**

KWA...

VVU (Virusi vya Upungufu wa Kinga Mwilini)

HCV (Virusi vya Homa ya Ini C)

STIs (Maambukizi ya Zinaa - Maambukizi yanayosambazwa kwa njia ya ngono)



VVU ni Ni?

VVU ni virusi vinavyoshambulia mfumo wa kinga ya mwili wa binadamu. Ikiwa havitapatiwa matibabu, VVU hudhoofisha mfumo wa kinga kwa kuharibu seli zinazopambana na maambukizi. Udhaifu huu wa kinga husababisha mwili kushindwa kujilinda dhidi ya magonjwa mbalimbali. Matatizo yanayotokana na VVU yasiyotibiwa yanaweza kusababisha kifo.

HCV ni Nini?

HCV ni virusi vinavyoshambulia ini. Ini lina jukumu muhimu katika kusaidia mmeng'eno wa chakula, kuondoa sumu mwilini, na kusaidia damu kuganda. Ikiwa maambukizi ya HCV hayatatiwa, yanaweza kusababisha cirrhosis (kovu kwenye ini), saratani ya ini, na hata kifo.

STIs ni Nini?

STIs ni maambukizi yanayosambazwa kutoka mtu mmoja hadi mwingine kupitia ngono ya uke, ya njia ya haja kubwa, au ya mdomo. Aina tofauti za maambukizi ya zinaa hushambulia sehemu tofauti za mwili. Maambukizi haya yanaweza kusababisha magonjwa makubwa na hata kuhatarisha maisha.


Ni nani anapaswa kupimwa VVU, STIs, na HCV

**KUPIMWA NI
HATUA YA KWANZA
NA MUHIMU ZAIDI**



Watu wazima wote wanapaswa kupimwa VVU na HCV angalau mara moja katika maisha yao

Kulingana na tabia, baadhi ya watu wazima wanapaswa kupimwa mara kwa mara zaidi.



Unapaswa kupimwa kila unapokuwa na mwenzi mpya wa ngono

Ikiwa umewahi kushirikiana vifaa vya kutumia dawa (kama vile sindano au vifaa vingine vinavyopenya mwilini), unapaswa kupimwa VVU na HCV.



Matibabu ya VVU

Matibabu ya VVU ni yenye ufanisi kiasi kwamba yanaweza kupunguza kiwango cha virusi vya VVU mwilini hadi kiwango ambacho hakiwezi kuonekana kwa vipimo. Mtu mwenye kiwango kisichotambulika cha VVU mwilini hawezi kusambaza VVU kwa mwenzi wake.

Hii inamaanisha



Matibabu ya HCV

Matibabu ya HCV ni yenye ufanisi mkubwa na yanaweza kuwa rahisi kama kumeza dawa ya kila siku kwa muda wa wiki 8-12. Watu wengi hawapati madhara makubwa, na mara nyingi hawapati kabisa madhara kutokana na dawa hizi. Zaidi ya 95% ya watu wanaopokea matibabu ya HCV hupona kabisa!

Matibabu ya STI

Maambukizi ya zinaa (STIs) ya bakteria kama vile Klamidia, Kisonono, na kaswende yanaweza kutibiwa na kupona kabisa kwa kutumia antibiotiki. Maambukizi ya zinaa ya virusi yanaweza kutibiwa ili kupunguza dalili, lakini hayawezi kupona kabisa. Daktari anaweza kukusaidia kudhibiti maambukizi ya virusi na kukusaidia kubaki na afya njema!

**YOTE UNAYOHITAJI
KUJUA KUHUSU
KUJIKINGA DHIDI YA**

VVU, STIs, na HCV

Kuna njia nyingi za kujilinda dhidi ya VVU, maambukizi ya zinaa (STIs), na HCV. Tafuta mbinu zinazokufaa!

Kondomu kwa kinga dhidi ya VVU, STIs, na HCV

Kutumia kondomu za ndani, kondomu za nje, na/au oral dams kila mara unapofanya ngono kunaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kupata VVU, STIs, na HCV kupitia ngono.

PrEP kwa kinga dhidi VVU

PrEP, au kingakinga kabla ya kuambukizwa, ni dawa ambayo watu wanaweza kutumia ili kuzuia kupata VVU kupitia ngono (inafanya kazi kwa 99%) au kwa kutumia sindano za dawa (inafanya kazi kwa 74%).

PEP kwa kinga dhidi VVU

PEP, kingakinga baada ya kuambukizwa, ni mpango wa dawa unaotakiwa kuanza ndani ya saa 72 baada ya mtu kuhusiana na hali inayoweza kumuweka kwenye hatari ya kuambukizwa VVU. Kadri unavyoanza mapema, ndivyo inavyokuwa na ufanisi zaidi katika kuzuia kupata VVU.

SSPs kwa kinga dhidi ya VVU, STI, na HCV

SSPs, au Mpango wa Huduma za Sindano, hutoa vifaa salama kwa watu wanaotumia dawa kwa sindano ili kuzuia kusambaa kwa magonjwa ya kuambukiza. Mara nyingi pia hutoa huduma za kinga na matibabu!

Dawa ya Doxy PEP kwa kinga dhidi ya STI

Dawa ya Doxy PEP, au kingakinga baada ya kuambukizwa kwa kutumia doxycycline, inahusisha kutumia dawa ya doxycycline ndani ya saa 72 baada ya ngono bila kondomu ili kuzuia kusambaa kwa kaswende (syphilis), klamydia, na kisonono (gonorrhea).

Ninaweza kupata huduma wapi?

Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu vipimo na matibabu!

Idara za afya za mitaa pia hutoa vipimo vya bure na vya siri vya VVU, STIs, na HCV. Idara zote za afya hutoa matibabu ya STIs na nyingi hutoa matibabu ya HCV na VVU pia!

Skana au bonyeza ili kupata idara ya afya iliyo karibu nawe!

**ZUNGUMZA. PIMA.
TIBU.**

